

MGOMBA KUPALILIA

1. Mke ni nguo juweni, wahenga walishasema
Msitamani njiani, madada na kina mama
Wavikeni walo ndani, imara mtasimama
Mgomba kupalilia, wahenga walishasema
2. Msitamani vya watu, mpalilie vya kwenu
Ninasema ndiyo utu, mtapunguza fununu
Usimtake Sikitu, ndani wamwacha Tunu
Mgomba kupalilia, wahenga walishasema
3. Siwaletei hotuba, ukweli naelezea
Fikirini kina baba, hekima zitawajia
Muwaonyeshe mahaba, mabusu kuwarushia
Mgomba kupalilia, wahenga walishasema
4. Muwapambe wapambike, bustani ziwe mwiko
Kila leo ukumbuke, unaye aliye wako
Na pia uambilike, umjulie wa kwako
Mgomba kupalilia, wahenga walishasema
5. Yalo bora muwavike, watapendeza machoni
Wavae wapendezeke, mtafurahi rohoni
Uwazi nao muweke, mtoleane undani
Mgomba kupalilia, wahenga walishasema
6. Na mengi mtaya hepa, nyumbani mkitulia
Magonjwa ni chapachapa, virusi mshasikia
Mijini kuna mipapa, mingingi na changudoa
Mgomba kupalilia, mke ni yake mavazi
7. Mke ni yake mavazi, ujumbe nishafikisha
Msigeuzwe mabuzi, na ngozi wakakausha
Sijauleta unazi, maadili kukumbusha
Mgomba kupalilia, wahenga walishasema

Msanif Shaaban

S.L.P 2180335

DAR ES SALAAM, Tanzania.
